## HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 10/12/2021 KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA.**

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Elizabeth M. Gumbo | Mkurugenzi Mtendaji (W) | M/Kiti |
| 2. | Bw. Michael Tolage | Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi (W) | Katibu |
| 3. | Bw. Goodluck Malisa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maliasili (W) | Mjumbe |
| 4. | Bw. Sile Salmini | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara (W) | Mjumbe |
| 5. | Bw. Denis | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi (W) | Mjumbe |
| 6. | Bw. Jordan Ojode | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango (W) | Mjumbe |
| 7. | Bw. Joshua S. Shayo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria (W) | Mjumbe |
| 8. | Bw. Harauna Taratibu | Afisa Habari (W) | Mjumbe |
| 9. | Bw. Robert Kibongolo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira (W) | Mjumbe |
| 10. | Bw. Jonathan J. Buluba | Mratibu wa Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W) | Mjumbe |
| 11. | Bw. Josiah Msiba | Afisa Biashara (W) | Mjumbe |
| 12. | Bw. Joshua Kelly | Kny.Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W)Mjumbe | |
| 13. | Bw. Msese K. Msese | Mwenyekiti wa Timu ya Mapato (W) | Mjumbe |
| **14.** | Dr. Kiraba Msoke | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 15. | Bw. Juma Joseph | Afisa Mipangomiji (W) | Mjumbe |
| 16. | Mwl. John Pamwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi (W) | Mjumbe |
| 17. | Bi. Amina Mbwambo | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (W) | Mjumbe |
| 18. | Eng. Furaha Mwampulo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (W) | Mjumbe |
| 19. | Bw. Erck | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA (W) | Mjumbe |
| 20. | Dr. Anold Msiba | Mkuu wa Idara ya Afya (W) | Mjumbe |
| 21. | Bw. Ngeleja Robert | Karani wa Kamati za Kudumu | |
| 22. | Bw. Malula M. Gogadi | Karani wa Kamati za Kudumu/Kaimu A/Uchaguzi | |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Filbert Kanyilizu | Katibu Tawala (W) |
| 2. | Mwl. Mtobi K. Edward | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari (W) |
| 3. | Bw. Mateso P. Kaswanu | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji (W) |
| 4. | Bw. Hagai Usiri | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki (W) |

**MUHT.CMT NA 01/06/12/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu wa kikao aliwajulisha wajumbe kuwa kwa mujibu wa kitabu cha Mahudhurio akidi ya wajumbe ilikuwa imetimia. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 07:00 mchana kwa kuwataka wajumbe kujadili kwa makini agenda zilizoandaliwa.



Scanned with CamScanner

**MUHT.CMT NA 02/06/12/2021: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Katibu wa Kikao aliwasilisha agenda za kikao kama ifuatavyo:

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda za Kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha Tarehe 11/11/2021
4. Yatokanayo na Muhtasari wa Kikao cha Tarehe 11/11/2021.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mwezi Novemba, 2021.
6. Taarifa ya Miradi ya Utekelezaji wa Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya na Ujenzi wa Miundombinu katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.
7. Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023
8. Taarifa ya Mapokezi ya Tsh.390,000,000.00 za Ujenzi wa Majengo ya EMD na ICU
9. Taarifa ya Miradi ya TASAF kila Kata
10. Taarifa ya shughuli za Kilimo mwezi Novemba, 2021
11. Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 23/11/2021
12. Kuahirisha kikao.

Wajumbe waliunga mkono agenda hizo zijadiliwe kama zilivyoandaliwa.

**MUHT.CMT NA 03/06/12/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 11/11/2021.**

Muhtasari ulisomwa mbele ya wajumbe, Muhtasari ulipokelewa na kuongezwa jina la Bw. Goodluck Malisa kwa wajumbe waliohudhuria kikao ambalo lilisahaulika kwenye orodha ya wajumbe waliohudhuria kikao. Baada ya marekebisho hayo wajumbe waliunga mkono kuwa muhtasari ni sahihi, hivyo ulitiwa saini na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe 07/10/2021.

**MUHT.CMT NA 04/06/12/2021: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 11/11/2021.**

**Azimio Na.1: Gharama za ujenzi wa uzio katika maeneo ya minada ya Laini na Migato zirekebishwe.**

Ilielezwa kuwa tathimini ya makisio ya ujenzi wa uzio kwenye minada ya Migato na Laini ulizingatia ukubwa wa maeneo hayo na gharama zilizoandaliwa zipo sahihi, vinginevyo ishauriwe kuyapunguza maeneo ya minada hiyo kama Halmashauri haina uwezo wa kugharamia kiasi cha fedha kilichotolewa.

Katika majadiliano, wajumbe hawakuafiki maelezo yaliyotolewa na kuliagiza gharama za ujenzi wa uzio katika Mirada ya Laini na Migato zirekebishwe.

**Azimio Na.2: Mhandisi wa Ujezi afuatilea kupata michoro ya majengo ya nyumba za watumishi OR-TAMISEMI kupitia taarifa zilizotolewa kwenye magroup ya Wakurugenzi Watendaji ili isaidie kuandaa makisio ya ujenzi wa nyumba za watumishi za gharama ya Tsh.50,000,000/= kwa kila nyumba.**



Scanned with CamScanner

Ilielezwa kuwa ufuatiliaji ulifanyika. Hata hivyo michoro iliyopatikana bado ina gharama kubwa kuliko kiasi cha fedha kilichopengekezwa cha kujenga nyumba ya mtumishi kwa gharama ya Tsh.50,000,000.00. Vinginevyo ishauriwe kupunguza ukubwa wa vyumba ili kupunguza vifaa kwenye manunuzi na gharama za ufundi.

**Azimio Na.3: Mpango kazi wa uandaaji wa anwani za makazi uwasilishwe katika kikao kijacho ili usaidie katika masuala ya ufuatiliaji.**

Ilielezwa kuwa azimio lilitekelezwa. Mpango kazi wa shughuli za uandaaji wa anwani za makazi utawasilishwa katika kikao hiki.

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Kamati ya wataalam Halmashauri ya wilaya ya Itilima wanaoshughulikia utekelezaji wa zoezi la uwekaji wa mfumo wa anwani za makazi na postikodi kwenye mitaa kama ilivyoelekezwa kwenye Mwongozo wa uanzishwaji wa Mfumo Anwani za Makazi na Postikodi wa mwaka 2016 wanaendelea na utekelezaji katika kata ya Lagangabilili ambayo ndiyo makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Itilima.

Ilifafanuliwa kuwa maandalizi ya ramani za mitaa inaendelea kupitia Idara ya ardhi, aidha, tarehe 07/12/2021 wajumbe wa kamati walihudhuria kikao cha maendeleo cha kata ya Lagangabilili ambapo taarifa ya uanzishwaji wa zoezi la uwekaji wa mfumo wa anwani za makazi na Postikodi iliwasilishwa.

Aidha sambamba na taarifa hiyo iliwasilishwa orodha ya wajumbe wa kamati pamoja na mpangokazi wa utekelezaji wa mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi Halmashauri ya wilaya ya Itilima kama inavyoonekana kwenye kiambatisho **A** orodha ya wanakamati, taaluma na wadhifa wake na kiambatisho **B** Mpangokazi wa utekelezaji wa zoezi la mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi Halmashauri ya wilaya ya Itilima.

**KIAMBATISHO A: ORODHA YA WAJUMBE WA KAMATI**

1. Juma Joseph Fokasi – Afisa Mipangomiji (W) – Mwenyekiti wa Kamati
2. Eng. Furaha Mwampulo – Mhandisi Ujenzi (W) – Makamu Mwenyekiti wa Kamati
3. Joshua S. Shayo – Mwanasheria (W) – Katibu wa Kamati
4. Mwishauri M. Matuki – Afisa Tehama (W) – Mjumbe
5. Robert O. Kibongolo – Afisa Usafi na Mazingira (W) – Mjumbe
6. Pascal Q. Tatock – Afisa Takwimu (W) – Mjumbe
7. Haruna N. Taratibu – Afisa Habari (W) – Mjumbe
8. Like S. Urembo – Afisa Maendeleo ya Jamii – Mjumbe
9. Rajabu J. Siasa – Afisa Mipangomiji – Mjumbe
10. Emmanuel Y. William – Afisa Ardhi – Mjumbe



Scanned with CamScanner

Wajumbe walipongeza utekelezaji huo na kusisitiza mpangokazi uzingatiwe ili kazi ifanyike kwa ufanisi kama inavyotakiwa. Aidha kikao kiliagiza iandikwe barua ya kuomba kuanzisha Baraza la Ardhi la Wilaya na kuwasilishwa kwa Msajili wa Mabaraza.

**Azimio Na.4: Idara ya Mifugo na Uvuvi ifuatilie na kukusanya ushuru wa ukaguzi wa nyama na kuwaelekeza Maafisia Mifugo walioko vijijini kutoza ushuru wa ukaguzi wa nyama.**

Ilielezwa kuwa azimio lilitekelezwa. Barua Kumb.Na.GK.12/344/25 ya tarehe 15/11/2021 imeandikwa na kupelekwa kwa Maafisa Mifugo wote wanaokagua nyama machinjioni kuwataka wawe wanakagua nyama, wanakusanya ushuru wa ukaguzi na wanawasilisha fedha katika kasma husika. Na kwamba taarifa ya ukaguzi iwasilishwe Halmahsauri kila siku ya Alhamisi.

**Azimio Na.5: Mganga Mkuu, Afisa Mipango na Mweka Hazina wakae pamoja kupitia makisio ya chf, User Fee na NHIF.**

Ilielezwa kuwa azimio limezingatiwa, mapitio yalifanyika na marekebisho kufanyika.

**Azimio Na.6: Rejesta ya Madeni ya Halmashauri apatiwe Mkaguzi wa Ndani kwa ajili ya kuhakiki kutokana na hoja ya ukaguzi iliyoibuliwa.**

Ilielezwa kuwa azimio lilitekelezwa. Rejesta ya madeni ya Halmashauri amepewa Mkaguzi wa Ndani kwa uhakiki.

**Azimio Na.7: Pikipiki ya Zahanati ya Chinamili ambayo haijapata mtumishi wa kuitumia katika Zahanati hiyo ihamishiwe maeneo mengine yenye uhitaji.**

Ilielezwa kuwa baada ya ufuatiliaji, ilibainika pikipiki DFP 7578 ilifanyiwa matengenezo na inatumika kwa shughuli za kituo. Aidha nakala ya taarifa ya Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Zahanati Chinamili imeambatishwa.

**MUH.CMT NA 05/06/12/2021: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI NOVEMBA, 2021.**

Mweka Hazina wa Halmashauri kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Novemba, 2021 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:

## 1.0 MAPATO

### 1.1 MAPATO YA VYANZO VYA NDANI

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilikisia kukusanya jumla ya Tsh **1,487,035,716.00** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani kwa mwaka 2021/2022. Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2021 Halmashauri imekusanya kiasi cha **Tsh. 109,651,842.21** na hivyo kufanya mapato yote ya ndani katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Novemba 2021



Scanned with CamScanner

kuwa jumla ya **Tshs. 578,423,550.35** ambayo ni sawa na asilimia **39** ya makisio ya mapato ya ndani ya mwaka 2021/2022.

## 1.2 MAPATO YA FEDHA ZA MATUMIZI MENGINEYO (OC) NA MISHAHARA

Ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilikadiria kupokea fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo(OC) na ruzuku ya mishahara ya watumishi(PE) kiasi cha **Tshs.** 19,413,871,460.00. Katika kipindi cha mwezi Novemba 2021, Halmashauri imepokea fedha za ruzuku ya Matumizi Mengineyo(OC) na ruzuku ya Mishahara ya Watumishi(PE) jumla ya **Tshs. 1,471,410,399.00**. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo:-

| Na | MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 | POKELEWA JULAI - SEPTEMBA 2021 | POKELEWA OKTOBA 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ruzuku ya Matumizi Mengineyo(OC) | 1,526,830,001 | 608,558,998 | 31,978,249 | 40 |
| 2 | Ruzuku ya Mishahara(PE) | 17,887,041,459 | 7,172,033,750 | 1,439,432,150 | 40 |
| | **JUMLA** | **19,413,871,460** | **7,780,592,748** | **1,471,410,399** | **46** |

## 1.3 MAPATO YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

Ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilikadiria kupokea fedha za ruzuku ya Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Tshs. 11,818,159,629.00.** Katika kipindi cha mwezi Novemba 2021, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha **Tshs 2,018,212,371.33** kwa ajili ya kughamia shughuli mbalimbali za Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo:-

| Na | MAELEZO | MAKISIO | POKELEWA JULAI – OKTOBA 2021 | POKELEWA NOVEMBBA 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Elimu Bure – Msingi | 933,693,000 | 284,551,110 | 79,089,112 | 38 |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Elimu Bure Sekondari | 624,387,500 | 156,322,165 | 44,853,986 | 35 |
| 3 | Ujenzi wa Jengo la Dharura Hospitali ya Wilaya – Fedha za Uviko - 19 | 300,000,000 | - | 300,000,000 | 100 |
| 4 | Ujenzi wa Nyumba za Watumishi wa Afya – Fedha za Uviko -19 | 90,000,000 | - | 90,000,000 | 100 |
| | **JUMLA** | **1,948,080,500** | **440,873,275** | **513,943,098** | **49** |

## 2.0 MATUMIZI.

Ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwezi Novemba 2021, Halmashauri imetumia jumla ya **Tshs. 2,779,865,794.00** kwa ajili ya kugharimia Miradi mbalimbali ya Maendeleo, kulipa Mishahara ya Watumishi na kugharimia shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Halmashauri. Mchangunuo wa matumizi ya fedha hizi ni kama ifuatayo:-

- Matumizi ya Miradi ya Maendeleo - Tshs. 897,296,347.00
- Matumizi Mishahara ya Watumishi – Tshs. 1,439,432,150.00
- Matumizi Mapato ya ndani - Tshs. 93,376,696.00
- Matumizi ruzuku ya Matumizi Mengineyo - Tshs. 349,760,600.00

**Jumla** **Tshs. 2,779,865,794.00**

Hivyo, jumla ya matumizi yote ya Halmashauri katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Novemba 2021 ni **Tshs. 9,808,464,269.00** sawa na **27`%** ya makisio ya mwaka ya **Tshs. 36,290,309,768.00.**

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa. Katika majadiliano, kikao kiliagiza Mweka Hazina afuatilie ushuru wa pango la NMB na TANESCO.
Kuhusu ushuru wa pamba, kikao kilimtaka Afisa Kilimo afuatilie Makampuni ambayo bado yanadaiwa ushuru ili walipe madeni yao. Vilevile Afisa Mazingira alete mpango mkakati wa kufuatilia usafi wa mazingira kwa kuwa kifungu cha faini zitokanazo na usafi wa mazingira bado makusanyo yake yapo chini.

**MUHT.CMT NA 06/06/12/2021: TAARIFA YA MIRADI YA UTEKELEZAJI WA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19, MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA AFYA NA UJENZI WA MIUNDOMBINU KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI.**



Scanned with CamScanner

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilipokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 78 katika shule za Sekondari kwa ajili ya wanafunzi watakaoingia kidato cha kwanza mwaka 2022 na madarasa 4 kwa shule za Msingi 2 shikizi za Mawkimisha Kata ya Luguru na Nlagaswa katika Kata ya Nkoma.

Ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwanzoni mwa mwezi Desemba, 2021 sehemu kubwa ya ujenzi wa madarasa yalikuwa hatua mbalimbali za boma.

Pia ilitolewa taarifa ya hatua iliyofikiwa katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kanadi ambapo kuna miradi ya majengo mawili, moja jingo la maabara ambalo lilikuwa hatua ya ufungaji leta ya juu na jingo la wagonjwa wan je (OPD) ambalo lilikuwa hatua ya kufunga box kwa ajili ya mxingi na kumwaga jamvi.

Vilevile ilitolewa taarifa ya hatua iliyofikiwa ya miundombinu inayoendelea kujengwa katika Jengo la Utawala ambayo ni ujenzi wa uzio, ujenzi was too, ujenzi wa kalakana, ujenzi wa chumba cha jenereta pamoja ambayo miradi hiyo ilikuwa iko katika hatua mbalimbali pamoja na ujenzi wa tanki la kuvunia maji ya mvua ambalo lilikuwa imekamilika.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili. Baada ya majadiliano wajumbe waliunga mkono kuwa taarifa ni sahihi.

**MUHT.CMT NA 07/06/12/2021: TAARIFA YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI MWAKA 2022/2023**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima imeshaanza mchakato wa Bajeti mwaka 2022/2023 ambapo hatua za awali zimeshafanyika. Hivyo Kila Idara/Kitengo zilitakiwa kuandaa Mapngo na Bajeti wa mwaka 2022/2023 na kuwasilisha Idara ya Mipango ikiwa kwenye excel. Aidha Idara zenye vyanzo vya mapato nazo ziliagizwa kuandaa makisio ya mapato kwa mwaka 2022/2023 na kuwasilisha kwa Mweka Hazina.

**MUHT.CMT. NA. 08/06/12/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA TSH.390,000,000 ZA MAJENGO YA EMD/ICU**

Taarifa iliwasilishwa kwa wajumbe kwa kuelezwa kuwa Serikali imetoa Kiasi cha Tsh.390,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za dharura (EMD) wagonjwa mahututi (ICU) wodi ya wagonjwa ya mlipuko (treatment centre) na nyumba za watumishi kuwa ambapo ujenzi huo utatekelezwa kwa kutumia Wakandarasi.

Ilielezwa kuwa katika maelekezo hayo vilevile umetolewa mwongozo wa ununuzi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotolewa na IMF za Miradi ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 uliotolewa na PPRA Novemba, 2021.

Ilielezwa kuwa maelekezo yametolewa kuwa usimamizi wa miradi hiyo utafanywa na Wahandisi wa Halmashuri kwa kusaidiwa na Wahandisi wa Mkoa. Taratibu za kuwapata wakandarasi na kufanya taratibu za manunuzi ziwe zimekamilika ifikapo tarehe 31 Desemba, 2021 ili wakandarasi wakabidhiwe kazi.

**MUHT.CMT. NA. 09/06/12/2021: TAARIFA YA ,IRADI YA TASAF KILA KATA**

Mratibu wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) aliwasilisha miradi iliyoibuliwa na Jamii ambayo itatekelezwa kwenye vijiji kwa kutumia fedha za TASAF. Miradi hiyo ilionesha



Scanned with CamScanner

kila kijiji aina ya mradi uliopitishwa na gharama za utekelezaji. Hivyo kikao kiliwataka kila Mlezi wa Kata ahakikishe anafuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na isiwe kati ya Mratibu peke yake.

**MUHT.CMT. NA. 10/06/12/2021: TAARIFA YA SHUGHULI ZA KILIMO MWEZI NOVEMBA, 2021**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Idara ya kilimo umwagiliaji na ushirika kwa mwezi Novemba, 2021 imesimamia na kutekeleza kazi za usambazaji na ugawaji wa mbegu za pamba na alizeti kwa wakulima, usambazaji wa kamba za kupandia, kutoa elimu ya upandaji kwa kutumia vipimo sahihi kwa zao la pamba na mazao mengine, zoezi la upokeaji na ugawaji wa pikipiki kwa maafisa kilimo wa kata na vijiji, kutoa elimu juu ya kukabiliana na tishio la upungufu wa chakula, usimamizi wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia nafaka katika kijiji cha Ikindilo chini ya mradi wa TANIPAC pamoja na usimamizi wa vyama vya ushirika -AMCOS.

Kuhusu kilimo cha pamba, ilielezwa kuwa Pembejeo zilizotumika katika msimu wa kilimo uliopita zilikuwa mbegu aina ya UKM 08 zisizokuwa na manyoya tani 857.420, viuadudu ekapaki 297,445 na vinyunyizi 700 ambapo pembejeo zote zilisambazwa kupitia AMCOS na kutolewa kwa wakulima kwa mkopo.

katika kutekeleza lengo hilo Wilaya ya Itilima imepewa lengo la kulima jumla ya hekta **46,667** sawa na ekari **116,668** za pamba na kutarajia kupata wastani wa mavuno ya tani **70,000** ambayo yatafikiwa kwa kuzalisha kwa wastani wa kilo 600 kwa ekali tofauti na uzalishaji wa sasa ambao ni wastani wa kilo 180 hadi kilo 200 kwa ekari. Wilaya ilipokea na kusambaza kwa wakulima kamba za kupandia 6,000 zilizotolewa na bodi ya pamba.

Ili kufanikisha azma ya kufikia uzalishaji wa kiasi hiki kwa mwaka 2021/2022 ilielezwa kuwanWilaya imejiwekea mikakati mbalimbali ya usimamizi na ufuatiliaji hatua kwa hatua kupitia vikosi kazi ngazi ya kijiji, kata na wilaya kuwezesha wakulima kuongeza tija katika uzalishaji wa pamba kutoka uzalishaji wa kilo 180 hadi kufikia kilo 600 kwa ekari moja. Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2021 jumla ya tani **1,046** za mbegu za pamba zilikuwa zimesambazwa na kuuzwa/kukopeshwa kwa wakulima kati ya lengo la mahitaji ya **1,170** zinazohitajika kama ilivyoonyeshwa katika jendwali hapa chini.

Kuhusu Kilimo cha Alizeti ilielezwa kuwa Halmashauri ya wilaya ya Itilima inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti kutokana na uhitaji mkubwa wa mafuta kwa nchi na ukuzaji wa kipato kwa wakulima na kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri ya wilaya.



Scanned with CamScanner

Hivyo Kutokana na uhamasishaji uliofanyika, ilielezwa kuwa wakulima wengi walihamasika kulima alizeti katika msimu wa kilimo wa 2021/2022. Jumla ya wakulima 28,645 wanatalajiwa kulima alizeti, kati yao wakulima 10,721 wanatarajia kulima wastani wa ekari 30,000 kwa kutumia mbegu tani 60 ambazo zimepokelewa katika wilaya ya Itilima kutoka wakala wa mbegu Tanzania (ASA) na matarajio ya mavuno ni wastani wa tani **12,600** kama mchanganuo unavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini.

Kuhusu kukabiliana na tishio la janga la njaa kutokana na uhaba wa mvua uliojitokeza, Kutunza na kutouza ovyo chakula walichovuna msimu uliopita , hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi kutumia sehemu ya mapato waliyopata kutokana na mauzo ya pamba kununua akiba ya chakula, kuacha matumizi ya nafaka katika utengenezaji wa pombe za kienyeji, kuuza sehemu ya mifugo yao na kununua chakula kwa kipindi hiki ambapo bado kinaonekana kuwa na bei nzuri na kinapatikana, kulima mazao yanayostahimili ukame na yanayokomaa kwa kipindi kifupi hasa viazi vitamu (ili vikikomaa watengeneze michembe kwa wingi) pamoja na kulima pamba na alizeti kwa wingi kwani mazao haya yanauwezo mkubwa wa kustahimili ukame ukilinganisha na mazao kama mahindi.

**MUHT.CMT. NA. 11/06/12/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KIKAO CHA TAREHE 23/11/2021**

Utekelezaji wa maazimio ya kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 23/11/2021 uliwasilishwa. Wajumbe waliwataka wahusika kwenye maazimio hayo wahakikishe wameyajibu kwa ufasaha.

**MUHT.CMT. NA. 12/06/12/2021: KUAHIRISHA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kuahirisha kikao, Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kuwa na ushirikiano wakati wote wa kikao na kuiitiza maazimio kufanyiwa kazi. Kisha aliahirisha kikao saa 07:40 Mchana na kuwatakia wajumbe majukumu mema..

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| Leo tarehe....7/1/2022 | Leo Tarehe....07/01/2022 |
| Saini.................... | Saini.................... |
| Jina ....Michael Tobae | Jina ....Matis P Haswan |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |



Scanned with CamScanner